

## Kilicho ndani ya Kasha



Kiunzi cha Ukutani | Kifuniko cha Kurembesha | Mlingoti | Silikoni | Skurubu za Mashine za Kichwa cha Kifungoe za milimita 12 aina ya M6 (4) | Parafujo aina ya M10 (2) | Ufunguo wa Pembe Sita wa Milimita 4

## Zana Zinazopendekezwa



Keekee / Bisibisi ya Umeme | Msumari wa Keekee wa Milimita 6 (1/4") | Soketi Milimita 10 | Penseli



## 1 | **Pakua Programu ya Starlink**

Changanua msimbo wa QR ili upakue Programu ya Starlink.




setup.starlink.com




## 2 | **Tafuta eneo la kufunga**

Starlink yako inahitaji mwonekano wazi wa anga ili iweze kuendelea kuunganishwa na setilaiti zinaposonga juu. Vitu vinavyozuia muunganisho kati ya Starlink yako na setilaiti, kama vile tawi la mti, mlingoti, au paa, vitasababisha ukatizaji wa huduma. Tumia zana ya kizuizi iliyo kwenye Programu ili kuhakikisha umechagua eneo linalofaa la kufunga.



## 3 | **Funga ikiwa na Nafasi kati yake na Sehemu za Jengo**

Hakikisha eneo la kufunga linatoa nafasi ya kutosha kwa Starlink yako, ambayo inaweza kuhitaji kuzunguka ili ilinganishwe vizuri.



## 4 | **Pitisha Kebo Ndani ya Kiunzi**

Ingiza ncha ya Kiunganishi cha Performance ya kebo ya Starlink ndani ya shimo katika upande wa mlingoti na uielekeze juu ndani ya nafasi iliyo kwenye adapta.



## 5 | **Chomeka Kebo ya Starlink**

Fungamanisha ncha ya Kiunganishi cha Performance ya kebo ya Starlink iliyoonyeshwa kwa mkato mwekundu na uichomeke kwenye Starlink yako kwa kushikilia ncha ya plagi na kuingiza kabisa kwenye sahani.

Ikiwa kebo ya Starlink inahitaji kuondolewa, zungusha kola kinyumenyume kisha uvute ili uitenganishe na Starlink yako.




## 6 | **Funga Kiunzi cha Ukutani Kwenye Starlink**

Funga skurubu za mashine ulizopewa kupitia kiunzi cha ukutani ziingie ndani ya sehemu ya nyuma ya Starlink na ukaze skurubu nne ukitumia ufunguo wa pembe sita. Kaza skurubu kwenye kona zote 4 hadi bolti zifikie N-m 7 (lb-ft 5.2). Hakikisha kiunzi kimeunganishwa imara kwenye Starlink.





### 7 | **Tia Alama kwenye Matundu ya Kuelekeza**

Tia alama kwenye eneo la matundu mawili kwenye kiunzi chako cha ukutani ukitumia kitia alama. Weka mashimo moja kwa moja juu ya mhimili wa jengo ili kufunga Starlink yako vizuri.




### 8 | **Toboa Matundu ya Kuelekeza**

Toboa matundu hayo kwa msumari wa keekee wa milimita 6 (inchi 1/4).



### 9 | **Weka Kizibaji kisha Ufunge Kiunzi cha Ukutani kwa Skurubu**

Tia silikoni ndani na juu ya matundu. Funga kiunzi kwa kutumia skurubu ulizopewa.

## 10 | **Ingiza Starlink kwenye Kiunzi cha Ukutani**

Ingiza mlingoti kwenye kiunzi cha ukutani. Zungusha Starlink yako ielekee kwenye mwonekano wazi wa anga.



## 11 | **Pitisha Kebo Ndani ya Kiunzi cha Ukutani**

Pitisha kebo ya Starlink ndani ya shimo katika upande wa juu wa kiunzi cha ukutani.



## 12 | **Funga Kifuniko**

Funga kifuniko na upitishe kebo ndani. Unganisha kebo ya Starlink kwenye Kigawi Mahiri cha Umeme kisha uunganishe kwenye umeme.



## 13 | **Fungamanisha na Ufunge Starlink Yako**

Arifa kwenye Programu itaonyesha ikiwa unahitaji kuzungusha Starlink ili ifungamanishwe vizuri.

Bofya arifa ili kutumia zana ya kufungamanisha. Mara baada ya kufungamanishwa, kaza skurubu ya kidole kwenye mlingoti ili kuzuia mzunguko.

